UTANGULIZI

Wakati wa juma la kuomba na kufunga katika mwaka wa 1993, Bwana Yesu alifurahisha moyo wangu kwa neno ambalo limekuwa limekuwa elezo la umisheni maishani mwangu; **"Ni jengee kanisa ambalo litawaleta mamilioni katika uwepo wangu kwa neno na nguvu."**

Baadaye, nilianza kujifunza juu ya nguvu za Mungu kwa kutafiti vifaa vyote vinavyohusiana kwenye maktaba yangu binafsi hata na maktaba ya seminari ya nyumbani na mbali. Kwa unchunguzi nilitambua kuwa machache yaliandikwa juu ya somo kwa muda wa karibu karne moja. Mwishowe nilikuja kujifunza juuya jinsi watu waweza kuwa na nguvu za Mungu mwenyezi katika maisha yao ya kila siku, hivyo nina furaha kushiriki nawe kile ambacho Bwana ameweka moyoni mwangu juu ya somo hili la kuchochevu.

Kujumlisha kuongeza, **nguvu za Mungu ni kwa waumini wote katika Kristo.** Nineshawishika kuwa, vile siku ya kurudi kwake Yesu zinakaribia, Mungu anatafuta chombo chake cha maana katika kizazi hiki kama hajawai. Katika historia (2 Mambo ya Nyakati 16:9). Ikiwa unatamani kuwa mwanamume au mwanamke wakutumika naye, tafadhali soma ujumbe huu ambao waweza kubadilisha maisha yako. Maisha yako hayatakuwa hivyo, mara tu utaposoma kuwa nguvu za Mungu zipo **kwako** leo!

Ni ombi langu la upole kuwa Mungu atatumia ujumbe huu kuleta njia mpya ya upako juu ya mwili wa Kristo; na kuleta ushindi kwa wale ambao wameshindwa na nguvu za giza, na kuleta mamilioni uweponi mwake, ambapo furaha ya kweli na milele kwa watu wote wangojao.

NGUVU

Baada ya miaka ya huduma ya nguvu na majaribio ya kurekebisha tabia, Mungu alinifunulia siri ya ukweli huu rahisi. **Ni kwamba nguvu za Mungu zimo katika uwepo waue.**

"Lakini mtapokea nguvu, akisha kuwajia juu yenu Roho Mtakatifu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika uyahudi wote, na Samaria na hata mwisho wa nchi (Matendo 1:8)**."**

Hili ni neno la mwisho (mapenzi) la Yesu Kristo kabla hajaenda mbinguni baada ya huduma yake ya duniani ya miaka 33½. Kulingana na kifungu hicho, tutapokea nguvu kama jibu la uwepo wa Roho Mtakatifu ikija kwetu. Ni wapi ulimwengum ambapo tunaweza kupata uwepo wa Roho Mtakatifu? Hapo ndipo palipo na uwepo wa Roho Mtakatifu! Ikiwa wewe ni mtu ambaye umezaliwa tena kwa maji na Roho, nguvu za Mungu zimo katika uwepo wake unaodumu ndani **yako**.

UWEPO

Ikiwa unatamani kuishi kama shahidi wa Kristo wa ajabu, ukiwa umejazwa Roho Mtakatifu na nguvu, ni muhimu kuwa unatembea **pamoja** na **ndani** na **karibu** na uwepo wa Mungu katika maisha yako ya kila siku. Kwa kuwa Mungu wetu ni mwungwana anayeheshimu jinsi tupendavyo kwa hiari. Inatupasa kuthibitisha ubwana wake kwetu na tukaribishe uwepo wake wa upendo katika njia zote maishani mwetu.

Biblia inasema katika Mwanzo 5:24, "Enoka alienda pamoja na Mungu naye akatoweka maana Mungu alimtwaa." Unapoamua kutembea katika uwepo wake wa ajabu na chini ya mwelekeo wake, mtiririko wa nguvu za Mungu ambazo zitakuwezesha kuwa shahidi wa ajabu na ishara kufuatia (Mariko 16:20) zitabalisha uungu wako kuwa kiumbe kipya. (2 Wakorintho 5:17). Kama jawabu kufuatia hili jambo la azili ambalo ni rahisi na la kushangaza, utaanza kuhisi uwepo wa Mungu katika njia ambayo hukuota kuwa yawezekana. Utagundua kuwa anatamani kuwa karibu nawe zaidi ya jinsi unavyotamani kuwa karibu naye.

GHARAMA

Hata hivyo, kuna gharama fulani ya kulipwa ili kupokea na kuweka nguvu za Mungu mwenyezi juu ya maisha yako.

1. GHARAMA YA MAOMBI: Ni muhimu **kulipa gharama** ya **maombi** ili utembee katika uwepo wa Mungu. Mwelekeo wa hema katika sura ya 9 ya waebrania inaonyesha mfano wa maombi yanayotuleta uweponi mwa Mungu. Biblia inatuambia kwamba ili kufikia patakatifu pa patakatifu ambapo uwepo wa Mungu unakaa, unapaswa upite madhabahu yashaba ukitoa maombi ya kutubu na, kutoa maombi ya kujisalimisha na mwisho, vifaa katika mahali patakatifu vinavyosimamia sifa na ibada. Hadi kufikia patakatifu pa patakatifu – kiwango ambapo utapewa nguvu kwa utukufu wake na wema – ni kuendelea kwa vita kinyume na nafsi! Lakini kumbuka **pasipo MAOMBI hapana NGUVU!**

2. GHARAMA YA MTU: Mara nyingi wakristo wanatazama zaidi, juu ya mojawapo ya mamilioni ya tabia za kristo, kama upendo wa Kristo, amani ya Kristo na baraka za Mungu na kadhalika. Hata hivyo, rafiki mpenzi, ni mara ngapi zaidi unafikiria, tunaweza kuguswa na kubarikiwa ikiwa tutakuwa wasikivu kwa **MTU** wa Yesu Kristo ambaye anamiliki yote, badala ya kumaliza muda wetu na nguvu zetu kushika tu kipande kimoja cha utu wake?. Hiyo ndiyo sababu Mungu wetu anajieleza kuwa **mimi ndimi** (Kutoka 3:14) ambayo inamaanisha kuwa ndiye kila kitu. Unachohitaji. Na huhitaji kutafuta msamaha, uponyaji, rehema, neema au baraka. Yesu ni yote jumla. Tafuta Yesu, si vitu ambavyo waweza kupata kwake! Wacha macho yako yawe kwa Yesu. Hii itafania uone kuwa mahitaji yako yanatimizwa.

3. GHARAMA YA KUTENGWA: Katika Hesabu 6:1-8, tunapata nadhiri yakutengwa kwa manadhiri watumishi wa Mungu waliotiwa mafuta, pamoja na yule Mungu ametenda kazi kuu katika historia ya Israeli. Yeyote anayetamani kutumika na Mungu lazima ajiweke safi na mtakatifu **kwa** kutoshika mke au mume asiyekuwa wake. **Kwa** kutokuza utukufu wa Mungu ambao ni wake Mungu pekee, na kwa kutokuza dhahabu, mali ya ulimwengu kando na baraka za Mungu katika maisha yake jinsi tu mnadhiri anavyopaswa kujiweka mtakatifu **kwa** kujinyima divai na kinywaji kingine kilichochacha**,** na kutokubali, wembe kupita kichwani pake, na kukaribia maiti. Ni kitu bora, naamini, kushikilia nguvu za Mungu juu ya maisha yetu kwa kujifia wenyewe kila siku kuwa chombo kilichotakaswa ambacho chaweza kuwa na uwepo wa Mungu ulio tajiri, na nguvu zake kuu, ijapo wengi wameanguka kwa kutojua jinsi ya kulipa gharama ya **KUTENGWA.**

KUHUSU MUANDISHI

- Mkurugenzi, EAPTC
- Alikuwa mwenyekiti, Glory Ministries in Kenya
- Mwanzilishi, ushirika wa The Power Army
- Oral Roberts University, USA

REV. P.S. LEE

Kwa maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na:

Paul Sungro Lee
Evangelical Alliance for Preacher Training & Commission

Kenya
King's Kids in Africa
P.O. Box 4871
Nairobi 00200

United States of America
P.O. Box 7, Merrifield, VA 22116

Republic of Korea
7-107 Miseong APT
Shincheondong, Songpagu, Seoul

Uganda
P.O. Box 1719, Mbale

Tanzania
P.O. Box 11484, Mwanza

Burkina Faso
B.P. 383, Koudougou

Internet
http://www.eaptc.org

E-Mail
eaptc@eaptc.org

Ujumbe huu waweza kutolewa katika njia yoyote bila kuvunja haki ya mwandishi. Tafadhali jisikie huru kuitumia katika njia yoyote kwa ajili ya faida ya mwili wa Kristo.

Imechapishwa Kenya

UEGUZWA NA UJUMBE HUU?

Mungu alinena kwa mchungaji Paul Sungro Lee wakati wa wiki ya kuomba na kufunga mwaka wa 1993; **"Nijengee kanisa ambalo litawaleta mamilioni katika uwepo wangu kwa neno na nguvu."** Tangu hapo, Mungu amemtumikia mchungaji Lee kujenga kanisa kupitia mafunzo ya Biblia, mikutano ya hadhara, mafunzo ya ukasisi, washa, matangazo redioni na uinjizlisti katika maandishi. Evangelical Alliance for Preacher Training & Commission (EAPTC), Glory Ministries in Kenya, King's Kids in Africa na ushirika wa The Power Army ni tunda la bidii kama hii.

Leo hii EAPTC inaendelea kufunza mamia ya wachungaji wenyeji wanaozalisha matunda na wamishonari kupitia kwa mpango wa shule ya umishonari iliyowekwa katika nchi saba (7) tofauti. Pia EAPTC na GMK unachunga zaidi ya makanisa 200 katika Kenya na Uganda (*yalioyohesabiwa tangu Januari 1, 2002*).

Ikiwa unataka kuwa mmoja wa huduma na kusaidia ujumbe huu wenye nguvu kuenea kujenga na kutia nguvu mwili wa Kristo ulimwenguni kote, tafadhali, toa cheti hiki cha chini na uitume kwetu. Tutakuwa na furaha kushiriki nawe kwa ajili ya kupanua ufalme wa Mungu.

"Niliguswa sana na ujumbe uliouandika ukiongozwa na Roho Mtakatifu."
-- Barua kutoka kwa kasisi Arthur Kitonga, Redeemed Gospel Church, Kenya

( ) Ndiyo, nitakuwa mmoja wa huduma yako kwa kukuombea kila mara.

( ) Ndiyo, nitasaidia ujumbe wa Nguvu kuenea katika jamii yangu kwa kutumika kama mpeperushaji wa kugawanya.
Nitumie nakala _____ za GHARAMA UWEPO NGUVU utoaji wa kugawanya.

( ) Tafadhali nitumie taarifa kuhusu ninavyoweza kununua kaseti ya audio ya GHARAMA UWEPO NGUVU, na ujumbe mwingine wa mchungaji Lee.
Lugha Inayopaswa: _____

TUMA KWA OFISI YA EAPTC ILIYOKARIBU NAWE.

Jina Lako _____

Anwani _____

_____

Simu _____

E-Mail _____

Ujumbe wa ubadilishaji maisha! Zaidi ya nakala 100,000 husambazwa na kusomwa ulimwenguu kote!

Gharama Uwepo Nguvu

Na Paul Sungro Lee